FUNZO LA 10

1. Ni ujumbe wa nani ulio wa muhimu sana duniani?
-Ujumbe wa Mungu.

2. Kwa nini ujumbe wa Mungu ni wa muhimu sana duniani?
-Kwa sababu wanadamu wote wamedanganya.
-Kwa sababu Mungu pekee hajadanganya.
-Kwa sababu Mungu pekee ndiye husema ukweli.

3. Je, kabla ya mwanzo nani pekee aliyekuwa hai?
-Mungu.

4. Je, Mungu alianza lini?
-Mungu hana mwanzo.

5. Je, Mungu aliumbwa na mtu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

6. Je, Mungu alijiumba?
-La.
-Mungu ni wa milele.

7. Je, mtu alimzaa Mungu?
-La.
-Mungu ni wa milele.

8. Je, Mungu alijizaa yeye mwenyewe?
-La.



-Mungu ni wa milele.

9. Je, kulikuwepo wakati ambapo Mungu hakuwepo?
-La.
-Mungu ni wa milele.

10. Je, Mungu hubadilika?
-La.
-Mungu habadiliki.

11. Je, Mungu anaweza kufa?
-La.
-Mungu hawezi kufa.

12. Je, Mungu ana nyama na mifupa kama watu?
-La.
-Mungu ni roho.

13. Watu wanahitaji chakula na maji, lakini Mungu anahitaji nini?
-Mungu haitaji chochote.

14. Kwa hivyo Mungu anaishi vipi?
-Mungu anaishi kwa nguvu yake mwenyewe.

15. Mungu yuko wapi?
-Mungu yuko kila mahali wakati wowote.

16. Kuna Mungu wangapi?
-Kuna Mungu mmoja tu.

17. Hao watatu ambao ni Mungu mmoja ni nani?
-Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu.

18. Nani aliumba mbingu na nchi?
-Mungu.

19. Mungu alitumia nini kuumba mbingu na nchi?
-Mungu hakutumia chocote.
-Mungu aliumba mbingu na nchi kutokana kisichokuwepo.

20. Mungu aliumbaje vitu vyote?
-Kwa kunena tu.

21. Mungu aliwezaje kuumba mbingu na nchi?
-Mungu ni mwenye nguvu zote.
-Nguvu za Mungu hazina mwisho.
-Hakuna asichoweza kufanya Mungu.

22. Mungu alijuaje jinsi ya kuumba mbingu na nchi?
-Mungu anajua kila kitu.
-Hekima ya Mungu haina mwisho.
-Hakuna asichoweza kufanya Mungu.

23. Mungu alisema nini kuhusu vyote alivyo viumba?
-Mungu alisema kila kitu ni kizuri.

24. Mungu aliwezaje kuumba kila kitu kikamilifu?
-Kwa sababu Mungu ni mkamilifu.

25. Ni nani Mungu aliumbia vitu vyote?



-Wanadamu.

26. Kwa nini Mungu akawaumbia wanadamu vitu vyote?
-Kwa sababu anatupenda sana.

27. Kwa nini Mungu ni mmiliki wa haki wa vitu vyote?
-Kwa sababu Mungu aliumba vitu vyote.

28. Kwa nini Mungu ana haki ya kutaka tuwe watiifu kwake?
-Kwa sababu alituumba na akatupa uhai.

29. Malaika wote walitoka wapi?
-Mungu aliwaumba.

30. Je, Mungu aliwaumba malaika na kuwapa nyama na mifupa?
-La.
-Mungu aliumba malaika kama roho.

31. Je, Mungu aliwaumba malaika wabaya na wazuri?
-La.
-Mungu aliwaumba malaika, wote wazuri.

32. Je, Mungu aliwaumba malaika kwa sababu alihitaji msaada?
-La.
-Mungu haitaji msaada.

33. Kwa nini Mungu aliwaumba malaika?
-Kwa sababu aliwapenda.

34. Hapo mwanzo malaika wote waliishi wapi?
-Mbinguni na Mungu.

35. Malaika wote wanaweza kuwa kila mahali wakati mmoja?
-La.
-Mungu pekee anaweza kuwa kila mahali wakati mmoja.

36. Jina la malaika aliyeumbwa na Mungu akiwa na hekima nyingi na urembo mwingi ni nani?
-Lusifa.

37. Siku moja hapo mwanzo Lusifa alifanya nini?
-Lusifa aliona hekima na urembo wake na akajawa na kiburi.

38. Lusifa alipanga kufanya nini?
-Lusifa alipanga kumtoa Mungu mamlakani.

39. Je, Mungu alimruhusu Lusifa kumtoa mamlakani?
-La.

40. Mungu alifanya nini alipokasirishwa na Lusifa?
-Mungu alimwondoa Lusifa mbinguni.

41. Mungu alifanya nini alipokasirishwa na malaika waliomfuata Lusifa?
-Mungu aliwaondoa mbinguni pia.

42. Jina jipya la Lusifa ni lipi?
-Shetani.



43. Jina "Shetani" linamaanisha nini?
-Linamaanisha "adui."

44. Jina jipya la malaika waliomfuata shetani ni lipi?
-Mapepo.

45. Mahali pa adhabu ambapo Mungu aliandaa kwa shetani na mapepo wake ni wapi?
-Ziwa la moto wa Milele.

46. Shetani na mapepo wake wanampinga nani?
-Wanampinga Mungu na kazi yake yote.

47. Baada ya Mungu kuiandaa nchi, alimuumba nani?
-Adamu, mwanadamu wa kwanza.

48. Mungu aliwaumbaje wanadamu na wanyama tofauti?
-Mungu aliwaumba wanadamu kwa mfano wake.

49. Inamaanisha nini kuwa Mungu aliwaumba wanadamu kwa mfano wake?
-Mungu aliwapa wanadamu akili wamjue.
-Mungu aliwapa wanadamu hisia wampende.
-Mungu aliwapa wanadamu mapenzi wamchague na wamtii.

50. Je, Mungu aliwaumba wanadamu wazuri au wabaya?
-Mungu aliwaumba wanadamu, wazuri pekee.

51. Mungu alimuumba Adamu na akampa mamlaka yapi?
-Mungu alimpa Adamu mamlaka juu ya nchi nzima na vitu

vyote ndani yake.

52. Baada ya Mungu kumuumba Adamu, alimuweka wapi?
-Katika bustani ya Edeni.

53. Jina la mti wa kwanza uliopandwa na Mungu katikati ya bustani ya Edeni ni lipi?
-Mti wa Uzima.

54. Kwa nini Mungu aliupanda mti wa uzima katikati ya bustani ya Edeni?
-Mungu alimtaka Adamu kula matunda ya mti huo na aishi milele.

55. Jina la mti ambao tunda lake Mungu alimwagiza Adamu asile ni lipi?
-Mti wa ujuzi wa Mema na Mabaya.

56. Kama Adamu angekula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya, nini kingemfanyikia?
-Adamu angekufa.

57. Kifo ni nini?
-Kutenganishwa na Mungu ambaye anapeana uhai.
-Kutenganishwa kwa nafsi na mwili.
-Kutenganishwa milele kwenye Ziwa la Moto wa Milele.

58. Mungu alimuumba nani kumsaidia Adamu?
-Mwanamke wa kwanza, Hawa.



59. Kwa nini Mungu alimuumba Hawa?
-Kwa sababu Mungu alimpenda Adamu.
-Kwa sababu Mungu hakumtaka Adamu awe peke yake.
-Kwa sababu Mungu aliwataka Adamu na Hawa wazae watoto.

60. Hapo mwanzo Adamu na Hawa walitembea na Mungu, na walikuwaje?
-Hapo mwanzo Adamu na Hawa walitembea na Mungu na walikuwa na furaha sana.